**USAFI, UZITO NA UKALI WA SHERIA YA NDOA**

*Na Christopher Mwakabanje*

"*Imenenwa pia, mtu akimwacha mkewe, na ampe hati ya talaka; lakini mimi nawaambia, kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini*" (Mt.5:31, 32).[1] Katika Marko 10:11,12 ametaja pande zote mbili, yaani mume na mke.

Yesu alikuwa akilinganisha haki ya Mafarisayo na ile ya injili. Katika Mishna, sehemu iitwayo Gittin, hutaja hati ya talaka ikijumuisha dhana aina tatu kutoka shule tatu za Kiyahudi; wakilitafsiri neno "ovu" katika Kumbukumbu 24:1 kwa mitazamo tofauti. Shule hizo ni: (1) Shammai, (2) Hillel, na (3) Akiba. (Petrillo, uk.69-70) [2]

Shule ya Shammai ilitafsiri neno "ovu" kuwa ni uasherati, sawa kabisa na Yesu alivyofundisha. Lakini shule ya Hillel ilifundisha kwamba ikiwa mke angeunguza hata mkate tu, basi angetalikiwa. Kwa hiyo, walilitafsiri neno ovu kuwa ni kosa lolote ambalo mke angekosa, ikiwemo hilo la kuunguza mkate, basi angetalikiwa na mumewe. Kadhalika dhana kutoka shule ya Akiba iliyodai kwamba neno ovu linalenga ukimwona mzuri kuzidi mkeo, basi hilo lilikupatia ruhusa ya kumtaliki mkeo (Petrillo).[3] Dhana zilizotajwa hapo juu zinathibitisha mitazamo ya Mafarisayo hata kuchukua hatua ya kumwuliza Yesu swali, "Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu?" (Mt.19:3).

Talaka iliruhusiwa na kuchukuliwa kiurahisi sana na Wayahudi chini ya Agano la Kale. Mtalikiwa alipewa hati iliyosomeka "Nenda, u huru kuolewa na yeyote" (Gittin 9:3) (Petrillo, 71). Kazi ya hati hiyo ni kumlinda mwanamke mtalikiwa asije akashitakiwa kuwa mzinzi mara aolewapo tena.

Kulingana na mafundisho ya Yesu, mke au mume hana ruhusa kumwacha mwenzi wake isipokuwa kwa UASHERATI. Hivyo basi, anatofautiana na mafundisho ya waandishi na Mafarisayo; akipinga talaka kutolewa kwa kila sababu, isipokuwa uasherati. Kulingana na Kamusi ya Vine neno uasherati limetafsiriwa kutoka neno la Kiyunani "porneia" lenye maana kitendo haramu cha kujamiana. Neno hilo linajumuisha uzinzi (kujamiana na asiye mwenzi wako wa ndoa), ufiraji, ulawiti, n.k.

Mungu aliiumba ndoa na kuitakasa ili katika hiyo aendeleze uzao wa binadamu. Ndoa inapaswa iheshimiwe na malazi (kitanda cha wanandoa) yawe safi; kwa kuwa Mungu atawahukumu wote wanaonajisi mpango wake wa asili wa ndoa (Ebr.13:4; Mt.19:4-6).

Katika Warumi 7: 2,3 Mungu anatoa ruhusa nyingine ya mtu kuoa/olewa tena nayo ni mwanandoa mmoja anapofariki dunia, aliye hai anaweza kuoa/olewa.

---

[1] Maandiko yote Yametolewaka *Biblia ya Union Version*, Isipokuwa Palipotajwa.
[2] Petrillo, Denny, CD Notes, World Video Bible School, Texas: Maxwell, USA 2003 pp. 69-70
[3] Petrillo, p. 71

Hivyo, ukiwa umeoa/olewa na mtu aliyeachwa pasipo sababu ya UASHERATI, basi unaishi katika uzinzi maisha yako yote. Usipoachana na ndoa hiyo na ukafa hali hiyo, basi utaangamia milele Jehanam.

Wengine wanapotosha neno "hafungiki" katika 1 Wakorintho 7:15. Watu hao, jambo la kushangaza, wanashindwa kuelezea mambo ambayo Paulo alifafanua wazi katika mistari 10 na 11. Paulo anasema huwezi kumlazimisha asiyeamini kuendelea kukaa na wewe ikiwa hataki kufanya hivyo. Mtu asiyejua usafi, uzito na ukali wa sheria ya ndoa hautamlazimisha aendelee kukaa naye ikiwa angehatarisha uhusiano wako na Mungu. Injili ilipofika mji wa Korintho (kama ilivyokuwa katika miji mingi ya Mataifa) wenyeji walikuwa wakiishi maisha ya kipagani. Mwanandoa mmoja alipoamua kuachana na maisha hayo na kuishi maisha safi ya Ukristo, hilo upande mwingine liliathiri mahusiano baina yao. Ebu, fikiria iwapo asiyeamini akaondoka, lakini baada ya muda akaamua kutii injili na kutaka kumrudia mumewe? *"Lakini wale waliokwisha kuoana nawaagiza; wala hapo si mimi, ila Bwana; mke asiachane na mumewe; lakini, **ikiwa ameachana naye, na ake asiolewe, au apatane na mumewe**; tena mume asimweache mkewe"* (mkazo ni wangu). Paulo hajasema hapo kwamba akishaondoka asiyeamini, wewe unaruhusiwa kuoa/olewa. Kuondoka kwa asiyeamini hakutoi idhini kwa anayeamini kuoa/olewa. Wote wanaofundisha hivyo wanaongeza katika neno la Mungu na watahukumiwa.

Kutozingatia usafi, uzito na ukali wa sheria ya ndoa kulimghadhibisha Mungu hata kuangamiza ulimwengu kwa gharika (Mt.24:38). Sote tunatambua pia moja ya sababu ya kuangamiza miji ya Sodoma na Ghomora ilikuwa ni masuala ya kutozingatia usafi wa ndoa (Mwa.19:5; Rum.1:24; Lk.10:12). Kanisa sasa linakabiliwa na changamoto nyingi hasa kutokana na suala zima la zinaa. Baadhi ya Wakristo kufikiria talaka ni suala la kawaida kabisa kwao! Mungu anachukia kuachana (Mal.2:16).

**kapalapala@yahoo.com**
**www.kanisalakristo.com**
**kanisalakristo@yahoo.com**